

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA NNE

27 APRILI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 27 APRILI, 2023

I. DUA:



II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

175. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Mfuko wa Taifa wa Watu wenyewe Ulemavu utaanza kufanya kazi.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

176. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa Afya na Elimu katika Jimbo la Igalula.

177. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itahuisha mpango wa upanuzi wa Manispaa ya Moshi kutoka Km 58 hadi Km 146 pamoja na kuwa Jiji.

178. MHESHIMIWA DKT. ALFRED JAMES KIMEA (KOROGWE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa Hospitali kongwe ya Magunga.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

179. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakarabati upya Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani Pemba pamoja na Nyumba za kuishi Askari wa Kituo hicho.

WIZARA YA NISHATI:

180. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme wa REA kwenye Vijiji 23 Wilayani Mkalama.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

181. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali italifanya Somo la Kilimo kuwa la lazima kwenye Vyuo vya Ufundu.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

182. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Kivuko kipyaa cha Kigamboni utaanza baada ya kutengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023.

183. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege Lindi kwa kiwango cha lami pamoja na kukarabati Uwanja wa Ndege Nachingwea.

184. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara ya Kigonsera hadi Mtiri na Mbinga hadi Litembo kwa kiwango cha lami.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MADINI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA
27 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**